

"Ujana hauna umri." - Pablo Picasso

# KIJANA WA MAARIFA

Jinsi kijana anavyoweza kuyamudu maisha ya dunia ya leo.

EDIUS KATAMUGORA


A young man with glasses and a beard is smiling while reading an open book in a library. He is wearing a white long-sleeved shirt. The background shows bookshelves filled with books, creating a warm and intellectual atmosphere.

"Ujama hauna umri" - Pablo Picasso

# KIJANA WA MAARIFA

Jinsi kijana anavyoweza kuyamudu maisha ya dunia ya leo.

EDIUS KATAMUGORA



# **KIJANA WA MAARIFA**

**JINSI KIJANA ANAVYOWEZA KUYAMUDU  
MAISHA YA DUNIA YA LEO**

**EDIUS KATAMUGORA**

Edius Katamugora 2020

## **Haki ya Kunakili**

Hakuna mtu yeyote anayeruhusiwa kunakili au kutoa kitabu hiki kopi bila idhini ya mwandishi labda pale kinapotumika katika nukuu ndogo ndogo.

Pia usimtumie mtu kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

## **Mawasiliano:**

**0764145476/0758594893**

**ekatamugora@gmail.com**

Kwa rafiki yangu Saada Mpandachalo ambaye amekuwa akinisisitiza muda wote kuandika kitabu hiki. Bila wewe nisingeandika kitabu hiki.

Kwa Dativa Matungwa, umekuwa mstari wa mbele kunishauri na kunipa msaada wa hali na mali katika kazi yangu ya uandishi.

# YALIYOMO

## UTANGULIZI

1. DUNIA INATAWALIWA NA WATU WENYE  
MAARIFA
2. MAISHA HAYAHITAJI WATU WEPESI WEPESI
3. KUJIFUNZA HUANZA PALE UOGA  
UNAPOKUFA
4. UKIJIFICHA NA FURSA ZINAJIFICHA
5. ACHA KUFANYA MAMBO KWA MAZOEWA
6. UKIFUNZA FUNDISHA
7. SHUKRANI NI JAMBO LA KUFANYIKA  
HARAKA
8. JIFUNZE ZIADI UONGEZE UZALISHAJI
9. AKIBA HAIOZI, WEKEZA UKIWA KIJANA

10. MITANDAO YA KIJAMII NI FURSA  
WANAYOITUMIA WATU WACHACHE
11. NYOTA YAKO ITAONEKANA TENA  
KABLA YA JUA KUZAMA.
12. TAZAMA KILE KISICHOFANYWA NA  
WENGINE NA KIFANYE
13. AMINI KILE UNACHOTAKA KUKIFANYA  
NA KIFANYE
14. MAUZO NI MOYO WA BIASHARA
15. WATU WATANIFIKIRIAJE  
INAKUCHELEWESHA
16. MWANZO MGUMU
17. KILA KITU KINAWEZEKANA KAMA  
UKICHEZA SEHEMU YAKO

18. MAENEO MATATU PESA ILIKOJIFICHA
19. MAISHA HUANZA PALE UNAPOZALIWA
20. KIJANA NA UAMINFU.



## UTANGULIZI

Toka zamani nilitamani kuwaandikia vijana wenzangu kitabu. Rafiki yangu Saada Mpandachalo akaniambia niandike kijana wa maarifa. Inawezekana kuna wakati Mungu anawatumia watu waje wakupe mawazo, nimetumia miaka mitatu sasa kuandika kitabu hiki.

Ni jambo la furaha kuona kitabu hiki kimekamilika.

Humu nimezungumzia changamoto ambazo vijana wanatakiwa kuzitatua. Mambo ambayo yanakwamisha vijana wengi katika dunia ya leo ndiyo hasa nimezungumzia.

Humu utajifunza kuhusu fedha, biashara, mahusiano, namna ya kuwa mtu wa hamasa. Karibia kila kitu

ambacho unatakiwa kukifahamu kwenye maisha kama kijana kimo humu.

Kitabu hiki kimebeba dhana kuu ya maarifa kwani binafsi naamini kuwa kijana mwenye maarifa ndiye atakayeweza kuiongoza na kuitawala dunia ya leo (utaona hili katika sura ya kwanza).

Kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wanalalamika kwamba hawaoni fursa za hela, katika kitabu hiki nimekuwekea maeneo matatu fedha ilikojificha.

Ukiyafahamu hautaomba tena pesa kwa mama yako au baba yako, sijui kaka, wala dada.

Vijana ni watumiaji wazuri wa mitandao, je mitandao inawafaidisha, utapata kujifunza mengi kupitia sura ya kumi ya kitabu hiki.

Nikuombe usome kurasa hadi kurasa ya kitabu hiki kwani yote yaliyoandikwa hapa yanagusa maisha yako.

Kitabu hiki ni majibu ya maswali mengi ambayo vijana wengi hujiuliza. Unatamani kuwa na maarifa yanaweza kukuvusha katika madaraja mbalimbali ya maisha. Kitabu hiki ni cha muhimu kusomwa na kila mtu ikiwa anatamani maisha yenye utimilifu. Ni muhimu kukumbuka maneno ya Pablo Picasso aliyesema, "Ujana hauna umri."

Yote Yakishasemwa, nikutakie usomaji mwema. Kumbuka pia kusoma vitabu vyangu kama vile Yusufu nina ndoto, Namna ya Kuwa Mtaalamu, Pumba za Edius na Natamani kuanza kusoma vitabu.

Edius Katamugora (24/6/2020)

## SURA YA KWANZA

### Dunia Inatawaliwa Na Watu Wenye Maarifa

Tupo katika kipindi ambacho kuwa na maarifa ni jambo la muhimu sana. Dunia ya sasa inatawaliwa na watu wenye maarifa. Bila kuwa na maarifa utajiweka katika wakati mgumu sana.

Maarifa yatakufanya uongoze kila unapokwenda, maarifa yatakufanya upendwe na watu, watu watahitaji kuwa karibu nawe muda mwingi. Maarifa yatakufanya uwe kinara, maarifa yatakufanya uwe mbobezi maarifa yatakufanya uitwe gwiji.

Magwiji wote ambao dunia ya leo inafurahia kazi zao walikuwa na wengine ni watu wenye maarifa. Vijana ambao wanafanya vitu ambavyo magwiji wa dunia walifanya binafsi nawaita *Vijana Wa Maarifa*.

Imesemwa mara nyingi kuwa, maarifa ni nguvu, maarifa huwa nguvu hasa pale yanapotumika. Kuwa na maarifa na yasitumike haiwezi kuwa nguvu bali ni hasara. Charles Darwin alikuwa sawa aliposema kitu kisipotumika kwa muda mrefu baadae hupotea au huishiwa nguvu. Hivyo maarifa yasipotumika nayo pia hupotea.

Maarifa ndiyo yametatua matatizo mengi yanayotuzunguka, maarifa ndiyo yametatua migogoro mingi katika jamii zetu, maarifa ni hekima. Wanasema hekima ni matumizi ya maarifa kutatua changamoto zinazotuzunguka. Watu wenye maarifa

katika jamii zetu ndio watu tunaowaona kama watu wenye hekima.

Watu wenye maarifa hutumia muda wao mwingi kufikiri namna ya kukumbana na changamoto mbalimbali na kuzitatua. Ni wazi kuwa kuna wakati unaweza kuona kitu kinafanyika mahali fulani na ukasema hata mimi niliwahi kufikiria kufanya jambo hilo lakini sikufikiria kama linaweza kuwa na matokeo makubwa kiasi hiki. Alichokuzidi huyu aliyeanzisha kitu hicho ni maarifa na taarifa. Wewe ulitaka kufanya kitu juu juu mwenzako alizama ndani na kuchimba zaidi.

Kama hauna maarifa, kama hautumia nguvu na hata kipato chako kuwekeza katika maarifa, jiandae kubaki nyuma siku zote. Wale unaowaona kila kukicha wanapiga hatua jua kwamba wamewekeza katika maarifa.

Tupo katika zama ambazo mashine zinakuja kwa kasi na kuondoa watu kazini. Kazi iliyoweza kufanywa na watu watatu ndani ya siku mbili inafanywa sasa na mashine moja, ndani ya saa kadhaa, kazi imekwisha. Kadri teknolojia inavyokua mashine nyingi zinaanza kufanya kazi za watu, hivyo kutakuwa na watu wengi sana wanaokosa kazi kwasababu kazi zao zitaanza kufanywa na mashine.

Hakuna asiyejua kwamba zamani ili ufanyiwe operesheni ulihitaji madaktari wasiopungua watatu, leo operesheni kama

hiyo inahitaji daktari mmoja, anayetumia muda mfupi. Mambo yamebadilika!

Ukiwa na maarifa katika kipindi kama hiki si rahisi kutoka kazini, ni wewe kujifunza kuendana na mifumo yake, wale ambao hawako tayari kujifunza maisha kwao yatawabadilikia. Uzuri ni kwamba mashine haiwezi kufikiri kama anavyoweza kufikiri mwanadamu mwenye maarifa, yenyewe imetengenezwa kwa mfumo wa kufanya kazi kwa namna fulani. Mtu mwenye maarifa mahali popote atategemewa kwasababu uwezo wake wa kuzalisha utakuwa mkubwa.

Kusema kwamba mashine zinawatoa watu kazini simaanishi watu walioajiriwa tu, hata wewe uliyeajiri kama hauna maarifa jiandae kuona biashara yako au kazi yako inakufa na inatawaliwa na watu wenye maarifa. Inafanya na watu kwenye viwango na ubora wa hali ya juu.

Siyasemi haya kumtisha mtu bali ni kujiandaa na yale yanayokuja mbele yetu. Lisemwalo lipo, kama halipo basi linakuja.

Kuna watu ambao wanafikiri kwamba wakimaliza shule mambo ya kujifunza yamekwisha wanasahau kwamba shule rasmi huanza pale wanapohitimu. Maisha ni shule ya kila siku. Hatupaswi kuacha kujifunza kwasababu maisha yenyewe huwa hayaachi kutupa mambo ya kujifunza.

**“Watu wengine wanakufa wakiwa na miaka 25 na hawazikwi hadi wanapofikisha miaka 75,”** alisema

Benjamin Franklin. Kuacha kujifunza ni sawa na kukaribisha kifo ukiwa bado hai, unakuwa mfu anayetembea (walking dead). Kuna ambao ni vijana na wameamua kuwa wazee na kuna wazee ambao bado ni vijana.

Kutokuwa na maarifa ukiwa kijana ni kujizeesha mapema, unakuwa umepitwa na wakati. Si jambo jema kama kijana kuitwa mtu aliyepitwa na wakati. Mambo yanapobadilika ni lazima na wewe ubadilike.

Wahenga walisema, **“Elimu ni bahari.”** Elimu haina mwisho. Jambo jema kuhusu maarifa ni kwamba yanapatikana kila kona, hayajifichi. Maarifa yapo vitabuni, maarifa yapo kwenye intaneti, maarifa wanayo watu ambao wanatuzunguka.

Ishi katika kutafuta maarifa, maarifa ni ufunguo wa mafanikio katika mlango unaoitwa maisha.